AFRO-ASIA YADAI MAMBO MATANO

Ngurumo 31/1/63

Uhuru uchumi bila minyororo, Ukoloni ukome, kudumisha kwa mila na starehe

MKUTANO WA AFRO-ASIA, UNATAZAMIWA KUHUDHURIWA NA WAJUMBE ZAIDI YA 400 KUTOKA PANDE MBALI MBALI ZA DUNIA, UTAFUNGULIWA NA RAIS WA JAMHURI YA TANGANYIKA MWALIMU, JULIUS NYERERE, TAREHE NNE MWEZI UJAO.

Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, Bwana Kambona, pamoja na Waziri siye Wizara Maalumu, Bwana Swai walikuwa mjini Moshi mwishoni mwa juma kumaliza mipango yote ya matayarisho ya mkutano huo kwa kushirikiana na wajumbe wa kudumu watakaoshiriki katika kuendesha mkutano huo.

Tarifa ya Serkali ilisema jana kuwa kwa muda wa wiki nzima hii, ndege zote zilizokuwa zinafanya kazi za uchukuzi kuwapeleka wajumbe huko Nairobi, zilikuwa zimejaa wajumbe wa mkutano huo. Hata hivyo juhudi zimefanywa kukodisha ndege nyingine kwa kukamilisha kazi hizo. Hotel zote mjini Moshi sasa zimejaa watu.

Agenda za mkutano huo tayari zimekwisha malizika kutayarishwa. Kuna mambo makubwa kabisa matano katika mkutano huo yatakayojadiliwa. Wakuu wa kila ujumbe, watakutana Jumaa Pili kuzichungua agenda na kuzichambua ikiwa ni lazima.

Jambo la kwanza litakalojadiliwa ni kutafuta uwezekano wa kulikuza shirika hilo la Afro-Asia ikiwezekana kujumlisha na nchi za Latini Amerika. Wasikilizaji wengine watatoka Cuba, kwa rais Castro, Brazil, British Guiana, Puerto Rico, na sehemu nyinginezo.

Ukoloni basi

Mkutano huo pia utajadili kwa nia moja 'kukomeshwa moja kwa moja kwa Ukoloni katika Bara la Afrika' na kuyafanya mataifa hayo yeheshimiwe na kujitawala haraka. Pia juhudi za kuwekwa kwa vituo vya kijeshi vya kigeni katika Ardhi ya Afrika kutakataliwa kabisa na mkutano huo pamoja na mikataba ya aina yeyote ya kijeshi. Mwisho, upasuaji wa mabom katika Afrika, nao utajadiliwa kwa kirefu.

Litakuja swala la uchumi. Hili litakuwa katika sehemu mbili. Uhuru kamili katika mambo ya uchumi kwa mataifa machanga na njia za kubadilishana katika mambo ya uchumi. Sehemu ya pili itakuwa ni kufikiria, Je, soko la nchi za Ulaya, Common Market, linaziumiza nchi zilizomo katika Afro-Asia ama la.

Agenda itakayofuata, [illegible] swala la mila. Nalo litakuwa katika sehemu mbili. Kudumishwa kwa Mila za Kitaifa. Kumaliza kabisa mabaki ya Ukoloni yenye nia za kupinga mila za Kitaifa.

Starehe

Mwisho kabisa litakuja swali la mambo ya starehe. Mkutano huo utalijadili kwa namna mbili, kwanza; mambo ya starehe kuhusu vijana na sehemu ya pili ni mambo ya starehe yanayowahusu akina mama.

Mkutano huo baada ya kufunguliwa na Rais zitasomwa salaam kwa Wakuu wa Nchi mbali mbali kwa watu na Katibu wake Mkuu.

Zikigongana

Katika mkutano huo, zitatumika lugha tatu, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili. Mkutano huo anatazamiwa kufanywa kwenye jumba la majengo ya secondary School katika shule ya Mawenzi ambako kutakuwa na wakalimani tayari kutafsiri lugha hizo zinapogongana.